BILL & MELINDA GATES foundation

Agosti 16, 2011

Mawasiliano:
Bill & Melinda Gates Foundation
Simu: +1.206.709.3400
Barua pepe: **media@gatesfoundation.org**

Shirika la Afrika Mashariki Lapokea Tuzo la Maktaba ya Kimataifa kwa Kutengeneza Vituo vya Elimu katika Maeneo ya Mashinani

Kitita cha dola milioni moja cha Ufikivu wa Tuzo za Elimu hutumika kwenye Mtandao wa Habari ya Maeneo ya Nchi Kavu katika kufikia habari na teknolojia kwenye jamii ambazo haziwezi kufikiwa kwa urahisi

SEATTLE – Wakfu wa Bill & Melinda Gates ulipeana leo Tuzo lake la mwaka wa 2011 la Ufikivu wa Elimu la dola milioni moja kwa Mtandao wa Taarifa katika Maeneo Kame (ALIN), inayotoa elimu na habari kupitia mbinu tofauti za idhaa za ubunifu kwenye jamii zilizo mashinani kote nchini Kenya, Uganda, na Tanzania. Wenyeji wa jamii hizi hutumia teknolojia na zana nyingine katika Vituo vya Elimu vya ALIN ili kupata habari katika kuimarisha afya yao, kuongeza mapato yao, na kuboresha maisha yao. Microsoft, ni mshiriki kwenye mradi kwa kusaidia maktaba ya umma kuunganisha watu walio na teknolojia na ujuzi unaofaa, itatoa msaada wa dola 270,000 kwa ALIN ili kugharamia programu na mpango wa mafunzo ya teknolojia ili kusaidia shirika hilo kuhudumia jamii za kawaida.

Vituo 12 mawasiliano vya ALIN—vinajulikana kama Vituo vya *Maarifa* —hulenga kutoa habari za utendaji wa moja kwa moja, hususan katika eneo la maendeleo ya kilimo. Idadi kubwa ya watu katika maeneo haya ni wakulima wa kilimo cha chini ambao wanahitaji habari kuhusu maswala kama vile kiangazi, wadudu, na kupata masoko ya kuuza mazao yao. Vituo hivi hutoa habari zinazolenga mahitaji bainifu ya jamii.

"Tunaelewa kuwa, kila jamii ambayo tunaihudumia ni tofauti, na kila mmoja tunaye mhudumia ni tofauti," James Nguo, mkurugenzi wa ALIN alisema hayo." Baadhi ya jamii zinahitaji habari kuhusu utekaji wa maji, bali nyingine zinashughulikia aina fulani ya wadudu. Pia tumegundua kuwa, watu wengine wanapojihusisha na maswala ya kompyuta na teknolojia, wengine wanapendelea kuishi katika mifano au mafunzo katika lugha yao asili."

Kuongezea kwa habari tunazotoa kwa wakulima, Vituo vya Maarifa huzungumzia maswala ya afya kama vile kijikinga na virusi vya UKIMWI na malaria, njia za kuimarisha maisha ya watu ya kila siku kama vile, jinsi ya kuunda jiko la gesi ya bayo, na maswala ya serikali kama vile kupata kitambulisho cha kitaifa au hali ya kuto tozwa ushuru. Watu wengine wametumia vituo hivi kuunda vikundi vya walemavu, kupata mafunzo zaidi mtandaoni, au kuunda biashara ya kiwango cha chini.

"Maelfu ya watu kutoka jamii hizi za mashinani ya Afrika Mashariki, wanaimarisha maisha yao kupitia habari zinazopatikana katika vituo hivi," Debora Jacobs, mkurugenzi wa uanzilishi wa

Maktaba ya Ulimwengu ya Wakfu wa Bill & Melinda Gates aliyasema hayo, kwenye hafla ya tuzo katika San Juan, Puerto Rico. “Wafanyakazi wote walio na ujuzi wanaweza kujifunza kutokana na modeli hii ya ubunifu ya kuafikia malengo, habari maalum.”

Vituo vyote vya Maarifa hutoa huduma ya bila malipo ya kompyuta na Mtandao na kutoa elimu ya bure jinsi ya kuzitumia. Kwa sababu, kunaye mwajiriwa mmoja tu anayelipwa katika kila kituo, ALIN hutegemea wahudumu wa kujitolea ili kusaidia kutoa huduma kuu. Wahudumu hawa wa kujitolea wanapokea mafunzo katika nyanja tofauti, pamoja na ujuzi wa kompyuta, mazoezi bora ya kilimo, matibabu ya hali ya ugonjwa, na ujuzi wa mawasiliano, mbinu hizi wanazitumia kuwafunza wengine katika jamii zao.

Kwa mfano, ALIN na wafanyakazi wa Kituo cha Maarifa cha Kyuso waliunda kikundi cha wakulima saba ili kushiriki kwenye mradi mkuu ambao uliwawezesha kusafiri katika maeneo mengine nchini ambapo wangeweza kujifunza mbinu za kudhibiti kiangazi, hali ya hewa ya ukame. Wakati wakulima walirejea Kyuso, walitekeleza mbinu hizo na waliweza kuimarisha kiwango cha mavuno yao. Wakulima walifanya kazi na waajiriwa wa Kituo cha Maarifa kuwafikishia wengine ubunifu wao, kupitia majaribio ya moja kwa moja, siku za nyanjani, videos, podikasti, na vipengee katika gazeti la ALIN Baobab. Mchungaji wa jamii aliweza hata kuhubiri kanisani mbinu hizo.

“Kutokana na taarifa ya Baobab na kwenye Kituo chetu cha Maarifa, niliweza kujua kuhusu utekaji wa maji. Nilijifunza zaidi kuhusu shughuli bora za kilimo kutoka maeneo mengine,” Ali Hassan Mulei, mmoja kati ya wakulima saba ambao walishiriki katika mradi huu mkuu, aliyasema hayo. “ Wakati wa kiangazi hupati chochote kutoka shambani. Lakini naenda shamba wakati wa kiangazi. Nachukua hela kidogo kutoka kwenye biashara yangu, naenda shambani, natengeneza mitaro, na kuunda misingi ya kuteka maji, na kisha na subiri kipindi cha mvua.”

Mradi wa Ufikivu wa Mafunzo ya Tuzo wa kila mwaka hutambua juhudi za ubunifu wa maktaba na mashirika husiani yalio nje ya Marekani katika kutoa ufikivu wa kompyuta na Mtandao bila malipo. Inatuzwa na mradi wa uzinduzi wa Maktaba ya Ulimwenguni, ambayo inawajibika ili kuimarisha ulimwengu wa elimu, habari, na nafasi ili kusaidia kuimarisha maisha ya mamilioni ya watu.

ALIN itatumia tuzo lake kupanua mtandao wake wa Vituo vya Maarifa, kupandisha daraja zanamango na zanatepe zake, kuongeza idadi ya kompyuta zinazopatikana kwa watumiaji wake, na kupanua mafunzo na elimu inayotolewa kwa waendeshaji wa mafunzo katika jamii. ALIN pia inaazimia kuunda kituo cha ubunifu ili kubuni mbinu katika habari na mawasiliano ya teknolojia.

###

Wakfu wa Bill & Melinda Gates
Unaongozwa na imani kuwa, maisha yana thamani sawa, Wakfu wa Bill & Melinda Gates unafanyakazi ili kuwasaidia watu wote kuishi maisha ya afya na ya kuzalisha. Katika nchi zinazokua, unalenga katika kuimarisha afya ya watu na kuwapatia nafasi ya kujijenga wenyewe kutokana na njaa na umaskini hohe hahe. Nchini Marekani, unahakikisha kuwa watu wote---hususan walio na rasilimali chache---wanapata nafasi wanazohitaji ili kufaulu shuleni na maishani. Makao yake yakiwa Seatle, Washington, wakfu unaongozwa na Mkurugenzi Jeff Raikes na Mwenyekiti William H. Gates Sr., chini ya maelekezo ya Bill and Melinda Gates na

Warren Buffett. Jifunze zaidi katika www.gatesfoundation.org au jiunge kwenye mazungumzo Facebook na Twitter.